Kwa Wanafamilia Wapendwa,

Kurasa zifuatazo zinakuonyesha jinsi ya kufasiri Ripoti ya Mwanafunzi Mahususi, ambayo inatoa muhtasari wa matokeo ya mwanafunzi katika mtihani wa hivi majuzi zaidi wa Tathmini ya Maendeleo ya Mwanafunzi wa Jimbo Lote la Iowa (ISASP). ISASP inanuia kutoa maelezo kwa familia kuhusu utendaji wa wanafunzi kulingana na Viwango Vikuu vya Masomo vya Iowa.

Katika ukurasa wa 1 wa ripoti, utaona muhtasari wa matokeo ya mwanafunzi wako katika jaribio la kila somo la ISASP. Kuna alama ya kipimo ya jaribio la somo, picha ya matokeo ya alama ya kipimo na kiwango cha mafanikio kulingana na alama ya kipimo. Kuna maelezo ya matokeo ambayo yanatoa maelezo zaidi kuhusu jinsi mwanafunzi wako anavyoelewa maudhui ya somo.

Katika ukurasa wa 2 wa ripoti, utaona matokeo ya mwanafunzi wako kwenye Nyanja Kuu za Iowa kwa kila jaribio la somo. Nyanja ni sehemu mahususi za maudhui ya kuzingatiwa ya somo. Kuna nyanja zilizoorodheshwa kwa kila jaribio la somo na asilimia ya maswali ambayo mwanafunzi wako alijibu kwa usahihi kwa kila nyanja.

Unapokagua matokeo ya ISASP, chukua muda wa kuzungumza kuhusu matokeo pamoja na mwanafunzi wako. Uliza maswali na upate maoni kutoka kwa mwanafunzi wako kuhusu sehemu za masomo aliyo na uwezo, usaidizi wa ziada unaohitajika na mambo yanayomvutia darasani. Wasiliana na shule yako kuhusu maoni na matokeo haya ya ISASP ili upate maelezo zaidi kuhusu jinsi ya kuendelea kumsaidia mwanafunzi wako katika ukuaji na fursa.

Wako Mwaminifu,

Mipango ya Majaribio ya Iowa

# ISASP
IOWA STATEWIDE ASSESSMENT of STUDENT PROGRESS

ISASP ni tathmini mpya ya jimbo lote inayolingana na Viwango Vikuu vya Iowa. Inatoa tathmini ya wazi na sahihi ya matokeo ya masomo ya mwanafunzi yanayohusiana na inayoweza kuchukuliwa hatua na wanafunzi, wazazi, waalimu na jimbo. Mwongozo huu unaelezea jinsi ya kusoma **Ripoti ya Mwanafunzi Mahususi**.

## *Ripoti ya Mwanafunzi Mahususi*
## *Ukurasa wa 1 kati ya 2*



ISASP
IOWA STATEWIDE ASSESSMENT of STUDENT PROGRESS

RIPOTI YA MWANAFUNZI

JINA LA KWANZA JINA LA MWISHO-ELAHISABATI SAYANSI
KITAMBULISHO CHA JIMBO#0123456789
JINA LA SHULE (5678)
JINA LA WILAYA (1234)

MAJIRA YA KUCHIPUA YA 2019 — GREDI YA 5

Jimbo la Iowa limejitolea kutoa tathmini ya ubora wa hali ya juu kwa wanafunzi wake. Tathmini ya Jimbo Lote la Iowa ya Maendeleo ya Mwanafunzi (ISASP) inalingana na Viwango Vikuu vya Masomo vya Iowa.

Matokeo haya yatawapa walimu, wazazi na wanafunzi maelezo muhimu kuhusu matokeo ya mwanafunzi ambayo yanaweza kutumika kuelekeza masomo ili kusaidia kila mwanafunzi kwa njia bora zaidi.

**Muhtasari kuhusu matokeo ya JINA LA KWANZA katika ISASP**

JUMLA YA SANAA YA LUGHA YA KIINGEREZA — Alama ya Kipimo: **475** — Kiwango cha Mafanikio: **STADI**



Jumla ya alama ya kipimo ya Sanaa ya Lugha ya Kiingereza (ELA) ni muunganisho wa alama zako za kipimo za Kusoma (999) na Lugha/Kuandika (999).

Mwanafunzi katika kiwango hiki ana maarifa, ujuzi na uwezo wa kuwa stadi katika ELA. Hii inaweza kujumuisha uwezo wa kusoma, kuelewa na kuchambua maandishi ya fasihi na maelezo. Hii inaweza pia kujumuisha uwezo wa kuandika vipande madhubuti ambavyo vinafaa, vyenye mpangilio na vinavyotumia Kiingereza cha kawaida. Ukurasa wa pili wa ripoti hii unatoa maelezo kuhusu matokeo ya mwanafunzi wako katika nyanja za ELA.

Maelezo zaidi kuhusu Jumla ya alama ya Sanaa ya Lugha ya Kiingereza ya mwanafunzi wako yanaweza kupatikana katika http://iowa.pearsonaccessnext.com/.

HISABATI — Alama ya Kipimo: **410** — Kiwango cha Mafanikio: **BADO SI STADI**



Mwanafunzi katika kiwango hiki hajaonyesha maarifa, ujuzi na uwezo wa kuwa stadi katika Hisabati. Ukurasa wa pili wa ripoti hii unatoa maelezo zaidi kuhusu matokeo ya mwanafunzi wako katika nyanja ya Hisabati.

Maelezo zaidi kuhusu alama ya Hisabati ya mwanafunzi wako yanaweza kupatikana katika http://iowa.pearsonaccessnext.com/.

SAYANSI — Alama ya Kipimo: **551** — Kiwango cha Mafanikio: **KIWANG[...]**



Mwanafunzi [...]a kiwango hiki ana maarifa, ujuzi na uwezo wa kuw[...] kiwango c[...]tika Sayansi. Hii ni pamoja na kutumia Mazoezi ya Sa[...]nsi na Uha[...] Maumbo pamoja na kuonyesha uelewa wa uchambuzi wa sayansi [...]mwili, dunia na anga. Mwanafunzi anawasilisha maoni na dhana za [...] kutumia mazoezi changamani ya sayansi. Ukurasa wa pili wa ripoti hii una[...]aelezo kuhusu matokeo ya mwanafunzi wako katika nyanja ya Sayansi.

Maelezo zaidi kuhusu alama ya Sayansi ya mwanafunzi wako yanaweza kupatikana katika http://iowa.pearsonaccessnext.com/.

http://iowa.pearsonaccessnext.com/
Ukurasa wa 1 kati ya 2 — mmddyy-Z00000000-12345678-00000000



* Kumbuka: Ikiwa huoni alama za jaribio lililoorodheshwa, tafadhali wasiliana na shule ya mwanafunzi wako kwa maelezo zaidi. Maelezo zaidi kuhusu ISASP na Ripoti ya Mwanafunzi Mahususi yanaweza kupatikana katika **http://iowa.pearsonaccessnext.com/**

### 1. MAELEZO YA MWANAFUNZI
Jina la mwanafunzi, Kitambulisho cha Mwanafunzi cha Jimbo la Iowa, shule, wilaya na gredi huonyeshwa katika sehemu ya juu ya ukurasa wa kwanza.

### 2. KIPIMO CHA MATOKEO
Kipimo cha Matokeo hutoa picha ya Kiwango cha Mafanikio ya mwanafunzi. Viwango vya alama kwa kila kiwango cha mafanikio huonyeshwa chini ya picha.

### 3. ALAMA YA KIPIMO
Alama ya Kipimo ni alama ambayo inaruhusu ulinganishaji katika gredi na miaka yote.

### 4. KIWANGO CHA MAFANIKIO
Kiwango cha Mafanikio kinaonyesha matokeo ya mwanafunzi kwenye jaribio na hutoa maelezo ya jumla ya kile ambacho mwanafunzi anafahamu na anaweza kufanya.

### 5. MAELEZO YA MATOKEO
Maelezo ya Matokeo ni ufafanuzi wa uelewa wa mwanafunzi kuhusu maudhui mahususi kwa kiwango cha gredi.

# ISASP IOWA STATEWIDE ASSESSMENT of STUDENT PROGRESS

## *Ripoti ya Mwanafunzi Mahususi*

## *Ukurasa wa 2 kati ya 2*



ISASP
MAJIRA YA KUCHIPUA YA 2019

GREDI YA 5

JINA LA KWANZA JINA LA MWISHO-ELAHISABATI SAYANSI
KITAMBULISHO CHA JIMBO# 0123456789

ALAMA KATIKA NYANJA

Alama katika nyanja zinaweza kutoa maarifa kuhusu uwezo wa mwanafunzi wako na fursa za kujiimarisha. Katika majedwali yaliyo chini ya alama katika nyanja za mwanafunzi wako zinaonyeshwa kama asilimia sahihi katika kila aina.

| Alama za Nyanja ya K[illegible]OMA-ELA | Asilimia Sahihi ya Mwanafunzi |
|---|---|
| Mawazo na Maelezo Muhimu | 82% |
| Usanifu na Muundo | 60% |
| Ujumuishaji wa Maarifa na Mawazo | 57% |

| Alama za Nyanja ya KUANDIKA-LUGHA-ELA | Asilimia Sahihi ya Mwanafunzi |
|---|---|
| Utafiti wa Kujenga na Kuwasilisha Maarifa | 37% |
| Uzalishaji na Usambazaji wa Uandishi | 83% |
| Aina na Mandhumuni ya Maandishi | 36% |
| Kanuni za Kiingereza cha Kawaida / Maarifa ya Lugha | 88% |
| Ufahamu na Matumizi ya Msamiati | 42% |

| Alama za Nyanja ya HISABATI | Asilimia Sahihi ya Mwanafunzi |
|---|---|
| Maarifa ya Shughuli za Kialjebra | 40% |
| Nambari na Shughuli za Msingi wa Kumi | 60% |
| Nambari na Shughuli - Sehemu | [illegible]0% |
| Vipimo na Data | [illegible]8% |
| Jiometriki | 57% |

| Alama za Nyanja ya SAYANSI | Asilimia Sahihi ya Mwanafunzi |
|---|---|
| Sayansi za Maisha | 84% |
| Sayansi za Kimwili | 92% |
| Sayansi za Dunia na Anga | 80% |



http://iowa.pearsonaccessnext.com/
Ukurasa wa 2 kati ya 2

### 6. NYANJA KUU ZA IOWA

Nyanja Kuu za Iowa ni maeneo mahususi ya kuzingatiwa ya yaliyomo na daraja ambayo yanajaribiwa. Kwa mfano, Mawazo na Maelezo Muhimu ni nyanja ya Kusoma katika gredi ya 5.

### 7. ASILIMIA SAHIHI

Asilimia Sahihi hutoa asilimia ya maswali ambayo mwanafunzi alijibu kwa usahihi katika kila Nyanja Kuu ya Iowa.

<u>ISASP hutathmini:</u>

- **Kusoma**
Kwa Gredi ya 3 - 11
- **Lugha na Kuandika**
Kwa Gredi ya 3 - 11
- **Hisabati**
Kwa Gredi ya 3 - 11
- **Sayansi**
Kwa Gredi za 5, 8 na 10

ISASP huwapa maelezo wanafunzi, wazazi, waalimu na jimbo kuhusu matokeo ya wanafunzi wa Iowa katika Viwango Vikuu vya Iowa. Imekusudiwa kutoa maelezo muhimu katika sehemu ambazo wanafunzi wanafanya vizuri na ambapo wanaweza kuhitaji usaidizi wa ziada. Wanafunzi na wazazi wanahimizwa kukagua matokeo kutoka kwenye Ripoti ya Mwanafunzi Mahususi na kuwasiliana na shule zao kwa maoni ya ziada.